




# Kadogo aenda shuleni



Tusome Early Literacy Programme

# Kadogo aenda shuleni



Kadogo alikuwa msichana yatima wa umri wa miaka saba.

Aliishi na shangazi yake katika kijiji cha Matemo.

Shangazi yake alikuwa maskini.  
Hakuweza kumpeleka Kadogo shuleni.  
Kila asubuhi Kadogo alienda mtoni kuchota maji.







Siku moja, mwezi wa Februari, Kadogo alikutana na chifu.

Chifu alimuuliza Kadogo kwa nini hakuwa shuleni.

Kadogo alimweleza kuwa yeye ni yatima. Alisema kuwa shangazi yake alikuwa maskini. Chifu aliahidi kumpeleka Kadogo shuleni.







Siku ya Jumatano, Kadogo na shangazi yake walienda ofisini mwa chifu.

Chifu alimnunulia Kadogo sare za shule. Baadaye alimpeleka hadi shule ya msingi ya Matemo.

Kadogo alifurahia darasa lake jipya.

Mwalimu aliwafunza siku za wiki, kuanzia Jumapili hadi Jumamosi.





Shangazi yake alisaidiwa na chifu kupata kazi.  
Alipata kazi katika shule ya Matemo.

Shangazi atapata pesa za kununua chakula na  
nguo.





Chifu alisema ni muhimu Kadogo aende shuleni kila siku.

Kadogo alifurahi sana na akasoma kwa bidii.

## Maswali

1. Kadogo alikuwa na umri wa miaka mingapi?
2. Kwa nini shangazi yake Kadogo hangeweza kumpeleka shuleni?
3. Kadogo na chifu walikutana siku gani?
4. Kadogo alipelekwa shule gani?
5. Kadogo alifundishwa nini shuleni?

# Kadogo aenda shuleni

Kadogo ni msichana wa miaka 7 lakini bado hajaanza shule. Anaishi na shangazi yake ambaye ni maskini. Siku moja anakutana na Chifu na maisha yake yanabadilika.



Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.